Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
Published on *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)

Ya Sayyidna Husaini

Kukuomba sina budi
Ya Razaku ya Wadudi
Ili utimu mradi
Yote nalo kusudia

Sikutaka kusimama
Mengi mno kuyasema
Ni mambo kunisukuma
Ni lazima kuelezea

Natokeza hadharani
Kwa ufupi nibaini
Yalomfika Husaini
Ya Rabbi niafikia

Yale ni mambo adhimu
Yalomfika Imamu
Sina shaka mwafahamu
Nami tawahadithia

Ule mwaka wa sitini
Wahijira sikieni
Kaondoka duniani
Muawiya kajifiya

Yazidi alitangaza
Nchi zote kaeneza
Dini ataiongoza
Ili watu kum-baiya

Barua aliandika
Madina kaipeleka
Kwa Walid ikafika
Nae akimwelezea

Kwa makini isomeni
Mfahamu yalo ndani
Kahitaji kura zenu
Isilamu wote pia

Nazidi kuyabaini
Yalio mwangu moyoni
Ni kura yake Husaini
Ufike kumwelezea

Husaini kastakimu
Akasema yakatimu
Huyo ni mtu dhwalimu
Kidini hakutimiya

Kama mimi ni haramu
Kukubali ya dhwalimu
Sitaki wake msemu
Mwambiye sitoridhia

Kwanza yeye nakiburi
Ni mlevi hana siri
Kajaa kila fujuri
Nyote mnamtambua

Sitokuwa chini yake
Hapa na pale afike
Taji hilo silo lake
Hata yeye yamwelea

Mtume alibaini
Kwa Hasani na Husaini
Ni Maimamu yakini
Kila mtu kasikia

Alfu kumi na mbili
Barua ziliwasili

Kwa mjukue Rasuli
Iraq zilitokea

Barua zilimtaka
Husaini huko kufika
Ukhalifa kuushika
Dini kuisimamia

Yazidi si mtu mwema
Sisi sote twafahamia
Na haya tunayosema
Wewe twakushtakia

Husaini hakutwawili
Katuma Ibn Akili
Ili kujua ukweli
Wa mambo yalomfikiya

Alipokewa vizuri
Wadogo hata kibari
Walimfanya safiri
Wa Husaini Msifiwa

Kisha mambo ligeuka
Balozi walimwepuka
Mapanga wakayashika
Muslimu kumuwa

Mwezi nane kutimia
Mfungo tatu sikia
Husaini kashika njia
Iraqi kaelekea

Naswaha zilimfika
Twakuomba kutotoka
Iraqi usije fika
Watu wakakukimbia

Husaini aliwambiya
Hayo yote nasikia
Nitakwenda nadhuria
Mtume kani uswiya

Wakiniuwa sijali
Aliniambiya Rasuli
Kua hayo majangili
Dhuluma watatumia

Alipofika njiani
Aliijua yakini
Ni hayuko duniani
Muslim kauwawa

Iraq waligeuka
Unafiki wakashika
Hivi waja kukushika
Husaini aliambiwa

Ule msiba adhimu
Ulomfika Imamu
Yeye na wake kaumu
Na kizaziche pamoja

Hapa ni pahali gani
Niambiyeni jamani
Ni Karbala jangwani
Husaini aliambiwa

Ibn Saad Omari
Na jeshile waliswiri
Maudhi na ujeuri
Imamu wamfanyia

Unyama walifanyiwa
Na kiu iliwauwa
Na maji kuzuiliwa
Hayo yote watendewa

Kauwawa Akbari
Pia hata Asghari
Na hao watu mashari
Mungu yuwashuhudia

Asghari ni kijana
Ni mdogo tena sana

Na kiu ilimbana
Kwa chembe walimuua

Husaini aliuliza
Fikirini mukiwaza
Kosa gani tulifanza
Kutendewa kama haya

Haya mambo ya huzuni
Alotendewa Husaini
Nashindwa kuyabaini
Ukumbuni kuelezea

Yangu haki mumetwaa
Ya ukhalifa sisawa
Na leo mwanisumbua
Nilipi mwafikiria

Au hamkusikia
Usemi wahashimia
Hapo akiwauswia
Kuhusu wake dhuria

Mama yangu ni Batuli
Binti yake Rasuli
Na baba yangu ni Ali
Waswii wake Nabia

Ya Husaini walimwaga
Damu yake bila woga
Walijifanya wajinga
Ufasiki mewashika

Kijukuu cha Rasuli
Ni Husaini bin Ali
Achinjwa kama ghazali
Wallahi twakulilia

Alipewa kila dhuli
Mwanao ewe Batuli
Ateswa na majangili
Wasio dini sikiya

Walisahau ahadi
Ya Mtume Muhammadi
Na wote ni mashahidi
Mtume akiwauswia

Alimchinja Husaini
Bila khofu na huzuni
Na Mungu si Athumani
Nae atamlipia

Ni kifo chenye kutisha
Tena kina babaisha
Wallahi cha huzunisha
Kila kinapo tolewa

Na Mungu si Athmani
Twalipiwa duniani
Wa kesho wenda motoni
Adhabu yawangojea

Hapo ndipo nitafika
Kalamu chini naweka
Kwa huzuni lonishika
Siwezi kuendelea

Mola atupe Imani
Yakumpenda Husaini
Tuwe nae na peponi
Dua zetu zipokea

Kisha Swala na Salamu
Zende hadi kwa Hashimu
Na alize Maimamu
Hasidi angachukia
.....

Source URL: https://www.al-islam.org/ar/node/40664#comment-0